



# Department of Justice

KWAAJILI YA KUTOLEWA KWA HARAKA  
ALHAMISI, 27 MEI, 2021  
[WWW.JUSTICE.GOV](http://WWW.JUSTICE.GOV)

CRT  
(202) 514-2007  
TTY (866) 544-5309

## **Idara ya Sheria Imekaa na Shule ya Wilaya ya Maine ili Kulinda Haki za Kielimu za Wanafunzi wenye Ulemavu na Wanafunzi wa Wanaojifunza Kiingereza**

### ***Mkataba Utakomesha Tabia ya Kimfumo ya Kufupisha Siku za Shule kwa Wanafunzi Wenye Ulemavu***

WASHINGTON – Leo Idara ya Sheria ilitangaza makubaliano ya suluhu na Shule za Umma za Lewiston kumaliza mfumo wa wilaya na tabia ya ubaguzi ya kuwatenga wanafunzi kutoka kwenye siku nzima za shule kwa sababu ya kitabia inayohusiana na ulemavu wao. Makubaliano pia yatahitaji wilaya kutoa fursa sawa za kielimu kwa wanafunzi wake wanaojifunza Kiingereza. Idara hiyo ilifanya uchunguzi wake chini ya Kifungu cha pili cha Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemavu (ADA, *Americans with Disabilities Act*) na Sheria sawa ya Fursa za Kielimu za 1974 (EEOA, *Equal Educational Opportunities Act*) baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Haki za Walemavu Maine (*Disability Rights Maine*).

Uchunguzi wa idara hiyo uligundua kuwa wilaya mara kwa mara ilifupisha siku ya shule kwa wanafunzi wenye ulemavu bila kuzingatia mahitaji yao ya kibinafsi au kutafuta msaada ambao utawawezesha kukaa shuleni siku nzima. Wilaya ina ukosefu wa mafunzo kwa wafanyikazi wake juu ya jinsi ya kushughulikia vizuri tabia za wanafunzi zinazohusiana na ulemavu hii ilichangia kutegemea zaidi kutumiwa kwa siku "zilizofupishwa" za shule. Wilaya hiyo iliongeza madhara kwa wanafunzi kwa kukosa kuwapa maagizo au msaada wa kitabia kipindi walipokuwa nje ya shule. Uchunguzi wa idara hiyo pia uligundua kuwa wilaya hiyo ilishindwa kutoa huduma stahiki kwa Wanafunzi wake wa wanaojifunza Kiingereza, ambao wengi wao walibaki katika mpango wa Wilaya wa Wanaojifunza wa Kiingereza kwa miaka mingi bila kuwa wajuzi wa Kiingereza. kwa matokeo hayo, wanafunzi wengi wa Kiingereza, ikiwemo wahamiaji na wakimbizi kutoka Somalia, Angola, na nchi zingine za Afrika, kukumbana na kuwa nyuma kielimu ambapo inaweza kuleta badhara baadae.

"Wanafunzi wenye ulemavu na wanafunzi ambao wanajifunza Kiingereza wanahitaji msaada wa ziada na huduma shuleni - sio vizuizi vya ziada vya kujifunza," alisema Mwanasheria Mkuu Msaidizi Kristen Clarke wa Idara ya Haki Kitengo Cha Haki za Kiraia. "Kuwapa wanafunzi wenye ulemavu nusu ya elimu wanayostahili haikubaliki. Kushindwa kuwahudumia vizuri watoto ambao wanajifunza Kiingereza hupunguza fursa zao za kufaulu katika shule yao ya sasa na baadae. Idara imejitolea kutekeleza sheria ili kuhakikisha shule zinakidhi mahitaji na zinaheshimu haki za wanafunzi wao wote."

"Tumetiwa moyo kwamba Shule za Umma za Lewiston zilishirikiana nasi katika uchunguzi wetu, zilitambua fursa ya kuboresha, na kujidhatiti katika kufanikisha utekelezaji wa makubaliano yetu," alisema Kaimu Wakili wa Marekani Donald E. Clark kwaajili ya Wilaya ya Maine. "Tunatarajia kufanya kazi na wilaya ili kuboresha fursa za elimu kwa wanafunzi wote."

Mwakili kutoka Idara ya Haki za Kiraia walifanya uchunguzi huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili wa Marekani kwaajili ya Wilaya ya Maine.

Utekelezaji ya Kifungu cha II cha ADA mashuleni na EEOA ni vipaumbele vya juu vya Idara ya Haki za Kiraia. Maelezo ya ziada kuhusu Idara ya Haki za Kiraia inapatikana kwenye tovuti yake ya [www.justice.gov/crt](http://www.justice.gov/crt), na taarifa zaidi kuhusu kazi ya Fursa za Kielimu inapatikana kwenye <https://www.justice.gov/crt/educational-opportunities-section>. Wanachama wa umma wanaweza kuripoti ukiukaji wa haki za raia kwenye <https://civilrights.justice.gov/report/>.

###

21-XXX

USIJIBU UJUMBE HUU. UKIWA NA MASWALI, TAFADHALI TUMIA MAWASILIANO KWENYE UJUMBE AU PIGA SIMU OFISI YA MAMBO YA UMMA KWA 202-514-2007.